JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

## TANGAZO

Tarehe 19/09/2022

**MWALIKO WA ZABUNI**

**ZABUNI NA. LGA/014/2022-2023/NC/11**

**UKODISHAJI WA ENEO LA BADECO (BEACH HOTEL) LILILOPO MTAA WA BADECO KATIKA KATA YA DUNDA**

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ya Bagamoyo anawatangazia Makampuni/ Taasisi/ Vikundi mbalimbali vya watu vilivyosajiliwa kisheria au Mtu binafsi,kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inakusudia kupangisha eneo la BADECO Beach Hotel (BAGAMOYO Development Corporation) kwa kuwekeza Huduma za kijamii na burudani. Huduma hizo ni kama, Huduma za chakula, Miundombinu mbalimbali kwa michezo ya watoto, Mabwawa ya kuogelea (Swimming pool), Huduma za vinywaji mbalimbali, Huduma ya eneo la kupumzikia wageni (Lodge) na shughuli zinginezo za burudani kulingana na matumizi ya Eneo kwa Mwekezaji.
Eneo hili lipo ufukweni mwa Bahari ya Hindi, ni eneo zuri kwa ajili ya uwekezaji wa shughuli mbalimbali za huduma za jamii na burudani. Eneo lina ukubwa wa ekari 1.88 sawa na mita za mraba 9,212 Eneo hili limegawanyika katika vitalu vyenye ukubwa tofauti ambavyo vimepangwa kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa.

Wawekezaji wote wenye sifa, nia na uzoefu mnakaribishwa kuomba kuwekeza huduma hizi za kijamii kwenye eneo la BADECO Beach Hotel.

### 2. SIFA/ MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI

i. Mwombaji anakaribishwa kutembelea eneo husika kwa ajili ya kujua na kuona mgawanyo wa Eneo kabla ya kuchukua na kujaza fomu. Siku ya kuonyeshwa eneo na wataalamu wa Halmashauri ni tarehe 22/09/2022 saa 3:00 Asubuhi.

ii. Mwombaji anapaswa kuwasilisha maombi kwa kujaza fomu ya maombi akiambatanisha na stakabadhi ya malipo ya Tshs. 20,000/= kama ada ya maombi ambayo haitarudushwa (non-refundable fund)

iii. Fomu za maombi zinapatikana ofisi ya Mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. na utapewa control namba kwa ajili ya kulipia ada ya fomu kiasi cha shilingi 20,000/=

iv. Mwombaji asiwe na mgogoro Halmashauri pia asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

v. Mwombaji awe na Leseni hai ya Biashara husika ambayo ataambatanisha nakara yake.

vi. Mwombaji aambatanishe nakara ya Namba ya Usajili wa mlipa kodi (TIN/VAT).

*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*
**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P. 59, BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.**
**Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz.** Tovuti:
www.bagamoyodc.go.tz

vii. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha nyaraka za kuonesha uzoefu wa biashara anayotarajia kuwekeza, uzoefu usiopungua mwaka mmoja.

viii. Mwombaji anatakiwa kujaza na kuwasilisha bei ya kukodi eneo kwa mita moja ya mraba (Square meter) kwa mwezi, kwa ajili ya kuwekeza katika kitalu/ vitalu vilivyoainishwa hapo juu.

ix. Muda wa uwekezaji utakuwa ni kuanzia mwaka mmoja hadi mitano. Kila mwombaji anatakiwa apendekeze muda atakaowekeza.

x. Mwombaji anatakiwa kuhakikisha anaanza uwekezaji ndani ya siku 60 kuanzia siku anapokabidhiwa eneo la kuwekeza.

xi. Mwombaji anatakiwa kuwekeza katika eneo hilo kwa kutumia miundo mbinu isiyo ya kudumu.

xii. Mwombaji anaruhusiwa kuomba eneo la uwekezaji zaidi ya moja endapo tu ataonyesha mpango kazi mathubuti wa kuendeleza maeneo aliyoyaomba.

**3.** Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni Ofisi ya Manunuzi (PMU) kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri siku za kazi.

**4.** Maombi yote yafungwe kwa lakiri na bahasha juu iandikwe

**UWEKEZAJI KATIKA ENEO LA BADECO BEACH HOTEL LILILOPO UFUKWENI MWA BAHARI YA HINDI WILAYA YA BAGAMOYO.**

Kwa anwani hii*:*

***KATIBU BODI YA ZABUNI,***
***HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO***
***S.L.P 59,***
***BAGAMOYO.***


**5.** Mwisho wa kupokea maombi haya ni saa nne (4) kamili asubuhi (saa za Afrika Mashariki) ya tarehe **03/10/2022 siku ya Jumatatu** katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea maombi mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochaguliwa kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

**6.** Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda uliopangwa kuisha, au yale yatakayotumwa kwa njia ya kierekitroniki hayatapokelewa na hayatafunguliwa.

Shauri Selenda
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**BAGAMOYO**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

TM/DPMO




MATUMIZI YA ENEO
1. VIOSKI 36 (Sqm 25)
2. GROCERIES 3 (Sqm 165)
3. BAR 3 (255 Sqm)
4. RECEPTION/OFFICE 1 (Sqm 57)
5. OSHEO LA MAGARI 1 (Sqm 110)
6. NYUMBA YA KULALA - 9 ROOMS
7. MAEGESHO YA MAGARI >100 cars
8. JENGO LA CHOO&BAFU 1 ( 16 Units)
9. MICHEZO YA WATOTO 1 ( Sqm 880)
10. SPACE ZA KUPUMZIKA 2 (360 Sqm)
11. BIASHARA NDOGO NDOGO 26 (Sqm 9)
12. MAENEO YA WAZI/Garden & Beach
13. BAR & COUNTER& SITTING SPACE 1

| Project | Client | Drawing title | LEGEND: |
|---|---|---|---|
| PROPOSED INVESTMENT PLAN TO BE BUILT AT PLOT NO.... BLOCK.. AT BADECO AREA.<br>-<br>BAGAMOYO - PWANI | BAGAMOYO DISTRICT COUNCIL,<br>P.O BOX 59,<br>BAGAMOYO - PWANI.<br>-<br>ded.bagamoyo@pwani.go.tz | BADECO - PROPOSED SITE PLAN<br>Date: August, 2022<br>Drawn by: Christina E S<br>Checked by: IDARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU MJINI NA VIJIJINI | Existing walls<br>Project number: BIP/001<br>Scale: 1:400 |

DISTRICT ENGINEER
BAGAMOYO